Wizara ya Elimu Sayansi na
Teknolojia na OR-TAMISEMI

GPE Transforming Education

# Programu

## YA KUIMARISHA STADI ZA KUSOMA, KUANDIKA NA KUHESABU





# UTANGULIZI


04: Programu ya GPE ilivyopeleka Tabasamu kwa Walimu, Wanafunzi

08: Madarasa ya mfano yanayoongeza kivutio wanafunzi wa awali

12: Wanafunzi wenye mahitaji maalumu walivyoguswa na mradi wa GPE

14: Programu ya GPE Ilivyoondoa changamoto kwa Taasisi za Umma, Shule za Msingi

16: GPE ilivyoongeza umahiri walimu, wawa kidigitali

18: Wadau wafurahishwa na utekelezaji wa mradi wa GPE

20: Serikali na wadau kufanikisha mafanikio ya elimu nchini Kupitia Programu ya GPE

24: Mchengerwa kulinda maslahi ya walimu

26: Wakuu wa Shule wasipokwe madaraka katika kusimamia miradi - Dkt. Msonde

28: Simamieni magari yaliyotolewa kufuatilia kazi za elimu - Mchengerwa

30: Sera mpya ya elimu, mtaala mpya kuleta mageuzi ya elimu Tanzania

32: “Serikali, Wadau nguvu moja kutekeleza Programu ya Kuboresha Kada ya Ualimu Tanzania (GPE TSP)”






Prof. Carolyn Nombo
Katibu Mkuu
Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia



Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa,
Adolf H. Ndunguru

# DIBAJI

Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia (WyEST) kwa kushirik iana na Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR-TAMISEMI) imetekeleza Mpango wa Stadi za Kusoma, Kuandika na Kuhesabu (KKK) kwa watoto wenye miaka kuanzia 5 hadi 13.

Mpango huu unalenga ufikiwaji wa Elimu kwa Watoto wote na ushiriki katika Elimu bora kuan zia ngazi ya Elimu ya Awali, Msingi, Elimu maalum na Elimu kwa walio katika mfumo usio rasmi hususan wanaotoka katika mazingira hatarishi na wenye uhitaji wa kupata fursa ya Elimu ya msingi.

Serikali inatotoa shukurani kwa wananchi na Wadau wa Elimu nchini hususani wazazi, wanafunzi, walimu, Kamati za Shule na Wathibiti Ubora kwa ngazi zote kwa kuboresha mazingira ya Ufundishaji na Ujifunzaji. Hii ni pamoja na ujenzi wa miundombinu ya elimu kwenye shule za msingi ambayo kwa namna moja au nyingine imechangia kuhakikisha hakuna mtoto anayeko sa fursa ya elimu.

Aidha, Serikali kwa namna ya pekee inawashukuru Wadau wa Maendeleo (The Global Partnership for Education-GPE) kwa kuendelea kuiunga mkono na kuweka tengeo la kiasi cha Dola za Kimarekani milioni 112.5 (sawa na shilingi za kitanzania 264,600,000,000.00 kwa kipindi cha miaka minne kuanzia 2019/2020 hadi 2022/2023. Fedha hii imechangia katika kuboresha mazingira ya ufundishaji na ujifunzaji ikiwa ni pamoja na ujenzi wa miundombinu. Hii imesaidia kuimarisha Stadi za Kusoma, Kuandika na Kuhesabu (KKK) hapa nchini.

Serikali inatarajia kuendeleza ushirikiano huu mzuri uliopo baina ya jamii na Wadau wote wa Elimu nchini ili kuboresha elimu na kuhakikisha elimu inatolewa katika ngazi zote.

**Prof. Carolyn Nombo**
**Katibu Mkuu Wizara ya Elimu,**
**Sayansi na Teknolojia**

**Adolf H. Ndunguru**
**Katibu Mkuu Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa**
**na Serikali za Mitaa**

# Programu ya GPE ilivyopeleka tabasamu kwa walimu, wanafunzi

WIZARA ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa kushirikiana na OFISI ya Rais-TAMISEMI imekuwa ikitekeleza program ya kuimarisha stadi za kusoma, kuandika na kuhesabu (KKK) kwa elimu wa msingi awamu ya pili (GPE-LANES II) ambayo inagharimu takribani kiasi cha Sh bilioni 264.6 za ufadhili wa Ushirika wa Kusadia Maendeleo ya Elimu (Global Partnership for Education - GPE).

Kazi nyingi zimefanyika ikiwa ni pamoja na ujenzi na ukarabati wa miundombinu kwa shule za msingi 1,449 ambapo jumla ya miundombinu 10,768 ambayo ni madarasa 2,980, matundu ya vyoo 7,673, nyumba za walimu 64, shule mpya 18 na majengo ya utawala 5.

Pia vifaa vya TEHAMA vimenunuliwa ikiwa ni pamoja na kompyuta za mezani 1,240, projecter 310, printa 310 na mashine za kudurufu 310 kwa ajili ya vituo vya walimu 459 kwa awamu ya kwanza nay a pili.

Kusini Mashariki, mradi wa GPE-LANES II umepeleka ahuweni katika sekta ya elimu kwa Wilaya za Masasi na Nanyumbu mkoani Mtwara.

Afisa Elimu Maalum Wilaya ya Nanyumbu, Ahmad Swaleh anasema Shule ya Msingi Chikotwa ni miongozi mwa shule zilizopokea fedha za program ya GPE-LANES, kati ya hizo Sh milioni 150 zimejenga nyumba za walimu na Sh milioni 40 zimejanga madarasa huku pia Sh milioni 400 zikielekezwa kujenga shule ya msingi mpya Kilimani Hewa.

"GPE-LANES imetusaidia pakubwa. Hapa Chikotwa hali ilikuwa tete, walimu walikuwa wanakaa umbali wa zaidi ya kilomita 3 kutoka kijiji jirani cha Chungu, lakini sasa mambo safi."

Mwalimu Mkuu wa Shule ya Msingi Chikotwa Suleimani Msami anasema: "kujengewa walimu nyumba kumewaondolewa walimu msongo wa mawazo uliochangiwa na kutembea umbali mrefu. Kwa sasa tuko shwari, tuko vizuri na tumechangamka na kuwa na furaha na tumekuwa na matokeo mazuri kwa wanafunzi wetu."

Mwenyekiti wa Kamati ya Shule ya Msingi, Chikotwa Juma Salileje anasema

**"GPE-LANES imetusaidia pakubwa. Hapa Chikotwa hali ilikuwa tete, walimu walikuwa wanakaa umbali wa zaidi ya kilomita 3 kutoka kijiji jirani cha Chungu, lakini sasa mambo safi.**





kukaa chini na umbali wa kilomita sita ulifanya wanafunzi wengi kuishia njiani na kuishukuru Serikali kwa kuitikia ombi la kuwapatia shule mpya.

Norasoli Similu mwanafunzi ambaye ni miongoni mwa walionufaika na ukarabati kwa kujengwa madarasa mapya kupitia mradi wa GPE-LANES awamu ya pili katika Halmashauri ya Wilaya ya Masasi anasema: "tunamshukuru Rais Samia kwani tulikuwa tunajazana, baada ya kujenga madarasa haya mazuri sasa wote tunatosha na tunasoma katika mazingira mazuri."

Wilaya ya Chato mkoani Geita nako mambo si haba, Mwalimu Mkuu wa Shule ya Msingi Magufuli, James Katwale anasema kupitia mradi huo wamejenga madarasa matatu kwa gharama ya Sh milioni 60 na ujenzi wa matundu matano ya vyoo kwa gharama ya Sh milioni 5.5.

"Programu hii imeweka mazingira mazuri yaliyosaidia kupunguza wanafunzi wasiojua kusoma, kuandika na kuhesabu, kwa kiasi kikubwa umetusaidia katika uimarishaji wa taaluma. Naishukuru Serikali na kama kuna fursa zingine zije ili tuendelee kuboresha elimu na watoto wasome kwa ukamilifu."

Katika Wilaya ya Ngara mkoani Kagera, mwalim wa Shule ya Msingi Munjebwe, Onesmo Kakoko anasema kujengwa kwa madarasa kumeongezea walimu hamasa ya kufundisha.

**Inaendelea uk 6**







# Programu ya GPE ilivyopeleka Tabasamu kwa Walimu, Wanafunzi

**Inatoka uk 5**

"Kupitia mradi huu tumebadilisha mazingira ya shule, tulikuwa na madarasa ya kizamani lakini sasa ni mapya, tunashukuru kwani maboresho yametusaidia watoto wawe na maendeleo mazuri ya masomo."

Mwalimu Mkuu wa Shule ya Msingi Kilombero, Yasini Nkala anabainisha kuwa wamepokea Sh milioni 400 kwa ajili ya ujenzi wa shule mpya ilioondoa msongamano kwenye shule mama ya Nyashahi.

"Tuna shule mama ya Nyashahi ambayo ilikuwa na wanafunzi takribani 3,000 kwa sasa wamehamishiwa Shule ya Msingi Kilombero, kupitia program ya GPE-LANES tumepata madarasa 11, ofisi za walimu, matundu ya vyoo zaidi ya 20 kwa ajili ya wanafunzi na walimu na nyumba za kisasa mbili zinazochukua familia mbili kwa nyumba moja."

Kuhusu nyumba mwalimu Hafla Makwara anasema: "nililazimika kutumia shilingi 3,000 kwa ajili ya bodaboda kwenda na kurudi kazini. Naishukuru Serikali kwasababu gharama ya usafiri imeondoa kwa kuishi karibu na shule. Naweza kuwasaidia watoto wasiojua KKK kuanzia saa moja asubuhi mpaka saa mbili ninapoanza vipindi rasmi vya darasani."

"Hivyo tunaendelea kuiomba serikali izidi kujenga shule na nyumba za walimu ili tuweze kutenda haki watoto wetu."

Ashura Chakupewa mkazi wa mtaa wa Kilombero wilayani Kasulu anasema kama wazazi wanafurahia ujenzi wa shule mpya ahatua ambayo imesaidia kuondoa msongamano madarasani na kuwaepusha wanafunzi na magonjwa ya milipo.

Katika kuimarisha ubora wa ufundishaji na ujifunzaji program ya GPE-LANES pia imewezesha Mafunzo Endelevu ya Walimu Kazini (MEWAKA) kwa kuwajengea uwezo walimu wa elimu ya awali, msingi, elimu maalum na ya MEMKWA.

Mafunzo hayo yamewafikia wawezeshaji wa kitaifa 195, viongozi wa elimu 984 na walimu wa elimu ya awali na msingi 26,657.

Afisa Taalum Manispaa ya Morogoro, Amani Mfaume anasema mafunzo ya MEWAKA yameongezea walimu umahiri na kuendelea kuzifahamu mada zilizokuwa changamoto kwao, hivyo kuwa na matokea makubwa na mazuri kwa watoto.

Mratibu wa Mafunzo Endelevu ya Walimu Kazini Morogoro, Rhoda Sheba anasema kupitia program ya GPE-LANES II vituo vya walimu vimeboreshwa na kuwekewa vifaa vya kisasa ambavyo vimesaidia walimu kujifunza kwa njia ya kidigitali.

Naye Rajab Mpela mwalimu shule ya msingi Kikundi mkoani Morogoro anasema vifaa vya TEHAMA vilivyowekwa kwenye vituo vya mafunzo vimesaidia ujifunzaji kwa njia ya vitendo.

Anasema vimesaidia walimu kuwa mahiri kwenye program mbalimbali kama program andishi na program jedwali (exel) ambazo zinamchango katika shughuli za kila siku za walimu.

"Kabla ya maboresho ilikuwa ngumu kufundishana mada zinazohusiana na TEHAMA na matumizi ya Kompyuta kwa walimu kwasababu tulikuwa tunasoma

> **"Kabla ya maboresho ilikuwa ngumu kufundishana mada zinazohusiana na TEHAMA na matumizi ya Kompyuta kwa walimu kwasababu tulikuwa tunasoma kwa nadharia kwa kuandikiana ubaoni.**






kwa nadharia kwa kuandikiana ubaoni."

"Mfano unapomfundisha mwalimu program jedwali (exel) katika kupanga matokeo ya wanafunzi ililazimu kufundisha kwa kuandika na kuchora ubaoni kitu ambacho kilikuwa kigumu kwa walimu kuelewa matumizi sahihi ya program."


Mwalimu wa Shule ya Msingi Konga, Gabriel Peter anasema mafunzo yamemsaidia ujuzi zaidi ikiwamo kupata mbinu mpya na hatua sahihi za kuwafundisha watoto wa dogo ili waelewe kwa Lugha ya Kiingereza.

Mwalimu Mkuu wa Shule ya Msingi Ukombozi, iliyopo Manispaa ya Singida, Yesaya Samweli anasema:"mafunzo yamesaidia wanafunzi wetu kupokea elimu na maarifa yanayostahili na kumuelewa vizuri mwalimu.

"Tumekuwa tukifundishana jinsi ya kuenenda na mada tata ambazo zinamfanya mwalimu ashindwe kufundisha vizuri na kushindwa kujiamini."

"Kwa program hii walimu wamekuwa mahiri na idadi ya wanafunzi hawajamudu stadi za kusoma, kuandika na kuhesabu ni kidogo sana na tunaamni ndani ya muda





mfupi wote watakuwa wanamudu stadi za KKK."

Mratibu wa MEWAKA Ngara Mjini mkoani Kagera, Emmanuel Bubelwa anasema vifaa vya TEHAMA vimerahisha mafunzo kwa walimu na kutoa matokeo chanya.

"Kwa sasa hatuna tena mfumo wa kutoa mtihani kwa kuandika ubaoni, wanafunzi wetu wamehama kwenye kufanya mtihani uliondikwa ubaoni kwa kufanya uliochapwa na ni kwa madarasa yote."

"Walimu wanakuwa wepesi kufanya kazi zao na hata mitihani ya mwisho wanafunzi wanafanya vizuri kwasababu wanakuwa na uzoefu wa kuona mitihani kwenye karatasi."

Mwalimu Mkuu Shule ya Msingi Tumaini Viziwi iliyopo manispaa ya Singida, Francess Edward anaishauri serikali kuongeza wigo wa program ya MEWAKA iwe endelevu na kuwafikia walimu wengi zaidi ili kuwaondoa walimu kufundisha kizamani na kwenda na wakati.

"Tunaishukuru serikali kwani program hii imekuwa na tija, tunaomba wigo uongezwe kwani walimu wanahitaji mafunzo ili wafanyekazi kwa ufanisi, dunia inaenda inabadirika na mwalimu wanapaswa wabadirike kama dunia inavyobadilika."







> Tuliamua kuleta mradi huu Shule ya Msingi Milola A kutokana na kuwa na idadi kubwa ya wanafunzi wa awali na yatasaidia kuondoa msongamano uliokuwapo mwanzo kutokana na shule kuwa na darasa moja lililokuwa dogo.

# Madarasa ya mfano yanayoongeza kivutio wanafunzi wa awali

KATIKA kuendelea kuimarisha elimu nchini, ikiwa ni sehemu ya utekelezaji wa Ilani ya Chama cha Mapinduzi, Serikali imechukua hatua mbalimbali ikiwemo kuimarisha mazingira ya ufundishaji na ujifunzaji kwa ngazi zote za elimu.

Kwa upande wa elimu ya awali ambayo ndio msingi wa elimu, Serikali kupitia Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia na Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa(TAMISEMI) inahakikisha kuwa kila shule ya msingi inatoa elimu ya awali kwa ufanisi katika mazingira na miundombinu iliyoboreshwa.

Mkurugenzi Msaidizi wa Elimu ya Awali na Msingi, Ofisi ya Rais-TAMISEMI, Suzan Nyarubamba Nussu anasema madarasa ya mfano ya awali yamejengwa katika shule za msingi 150 kwa awamu ya kwanza.

"Kwa awamu ya pili, pia shule za msingi 68 zinatarajia kupelekewa fedha kwa ajili ya ujenzi wa madarasa ya mfano ambayo yanazungumza."

Ujenzi wa madarasa ya mfano yanayozungumza ni sehemu ya utekelezaji wa mradi wa GPE-LANES II ambao umefadhiliwa na Ushirika wa Kusaidia Maendeleo ya Elimu (GPE) kwa gharama ya Sh bilioni 9.2.

"Mradi umefadhili mambo mengi kama madarasa haya(ya mfano), mabweni kwa ajili ya watoto wenye mahitaji maalum na madarasa ya kawaida shule kamili."

Afisa Elimu Kata ya Ikuti katika Halmashauri ya Rungwe mkoani Mbeya, Nsibwene Kaswaga anasema wamepokea fedha za kujenga madarasa mawili ya mfano ya elimu awali hatua ambayo imesaidia kupunguza mrudikano wa watoto madarasani.

"Pia tumepokea vifaa vingi ikiwa ni zana za kufundishia na vifaa vya michezo ya watoto ambayo havikuwepo, pia madawa ya watoto na magodoro kwa ajili ya watoto kupumzika na jambo lingine kubwa vyoo vya watoto





wadogo vimeboreshwa."

Kaimu Afisa Elimu Msingi Manispaa ya Lindi, Alex Mkwago anasema Shule ya Msingi Milora A, imenufaika na mradi huo baada ya kupokea Sh milioni 55.8 zilizotumika kujenga madarasa ya awali ya mfano, vyoo na vifaa vya michezo ya watoto.

"Tuliamua kuleta mradi huu Shule ya Msingi Milola A kutokana na kuwa na idadi kubwa ya wanafunzi wa awali na yatasaidia kuondoa msongamano uliokuwapo mwanzo kutokana na shule kuwa na darasa moja lililokuwa dogo."

Mwalimu Shule ya Msingi Milola A, Saud Rajab alisema: "kabla ya madarasa mapya tulikuwa na darasa halikuwa na mvuto kwa watoto, yaani haliongei, lakini kwa madarasa haya yanaongea na watoto wanafurahia hata utoro umepungua."

"Hata mimi linanipa hamasa ya kufundisha inavyotakiwa na ufundishaji wangu umekuwa rahisi."

Mwalimu Mkuu Shule ya Msingi Milola A, Imani Mohamed amesema walikuwa wanapokea wanafunzi wachache kutoka vijiji vitatu, wazazi walikuwa hawahamisiki kuleta watoto shule kutokana na jengo la awali halikuwa zuri, lakini sasa wamehamasika wanawaleta watoto wa awali.

Kwa upande wa Afisa Elimu Msingi Halmashauri ya Ruagwa, George Mbesigwe anasema Serikali kupitia program ya GPE LANES II imetupatia Sh milioni 55 kwa ajili ya ujenzi wa madarasa ya mfano kwenye shule ya msingi ya Chenjele

"Pia tuna mradi wa ujenzi wa shule mpya mbili ambazo zimejengwa kijiji cha Nandagala iliyotengewa shilingi milioni 400, na ya pili imejengwa kijiji la Likangara imesajiliwa mwaka 2023 imeanza na wanafunzi wa awali na wa darasa la kwanza."

Mzazi wa mwanafunzi wa darasa la awali katika Shule ya Msingi Namapoo, Arafat Mohammed ameshukuru watoto wao kusoma karibu na inakuwa rahisi kuwapeleka na kuwafuata wakati wa masika na wanafurahia kwenda shule.

**Inaendelea uk 10**









”

**Kwa kweli hata utaratibu wa uandikishaji watoto wanakimbilia kuleta watoto hapa shuleni na kuwatoa shule binafsi kutokana na mazingira jinsi yalivyo mazuri.**

**Inatoka uk 9**

Mwalimu Mkuu wa Shule ya Msingi Namapoo, Zuhura Makota anasema: “shule inapokuwa na wanafunzi wengi inampeleka mwalimu kuwa na kazi kubwa kuweza kumfikia mwanafunzi mmoja mmoja.”

“Mimi ni mwalimu wao na kupata shule mpya inanisaidia kuwafikia mwanafunzi mmoja hadi mwingine kwenye dawati, ninamfuatilia kwa karibu maendeleo ya mwanafunzi aliyeandika na asiyeandika naweza kumbaini na kutatua changamoto yake kwa mtoto mmoja mmoja.”

Anasema kwenye shule mama ilikuwa inapokea watoto zaidi ya 200 huku kukiwa na mwalimu mmoja, hivyo inakuwa ngumu kuwafikia kwa kipindi cha dakika 30.

Naye Mwalimu wa Shule ya Msingi Lukobe iliyoko Manispaa ya Morogoro, Agness Mgosha anasema mbali na kujengewa madarasa ya mfano pia kupitia mradi huo vimejengwa vyoo vya kisasa kuingana na jinsia zao za kike na wakiume.

Kwa upande wa mwalimu wa Shule ya Msingi ya Lukobe, Olimpia Mrema anasema:”michoro iliyochorwa darasa inawafurahisha watoto na kuwapa hamasa hata utoro umepungua na wengi wanafurahia kuja shule.”

Naye Afisa Slimu Kata ya Lukobe, Leonaled Mtete anasema awali wanafunzi wa awali walisomea chini ya mti na baadaye kwenye darasa ambalo halikuwa na mazingira mazuri.

“Baada ya kuwa kwenye mradi wa GPE LANES II tumepata madarasa mazuri na wanafunzi wanajifunza kwa vitendo na picha na kile mwalimu anaelezea wanakishuhudia na wanakiona.”

“Kwa kweli hata utaratibu wa uandikishaji watoto wanakimbilia kuleta watoto hapa shuleni na kuwatoa shule binafsi kutokana na mazingira jinsi yalivyomazuri.”

Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Shule ya Msingi Mikongeni Ukonga iliyopo Kata ya Gongolamboto, Mchungaji Richard Mtake anashukuru kwa ujenzi wa madarasa mawili ya awali kwani yametatua changamoto kubwa iliyokuwapo ya mrundikano mkubwa wa wanafunzi na nafasi ya kuwaweka ilikuwa ni ndogo.

“Lakini sasa mradi umetusaidia kwanza tumejenga madarasa mazuri, bora, kupendeza na kuvutia ambayo yamekuwa chachu ya kuwavutia wazazi na walezi kuwaleta watoto wao shuleni.”

“Kama kamati tulipopokea fedha za mradi na tulihakikisha haipotei hata senti, fedha ilisimamiwa kwa jinsi ilivyotakiwa na kila kitu kujengwa kwa ubora unaotakiwa.”

Naye Mwalimu wa Shule ya Msingi Mikongeni, Innocent Macha anasema mazingira mazuri ya madarasa hayo yanawavutia wanafunzi kuwapo katika maeneo ya shule kwasababu kuna vitu mbalimbali vinavyowafanya wao kuwepo hapa.

“Kwanza kuna madarasa mazuri, tuna bembea nzuri ambazo mtoto akisoma na kuchoka anaenda kumbembea, inamvutia mtoto kuja shule hata kama hapendi shule.”







“Hata ufundishji unakuwa rahisi maana situmii nguvu nyingi kwasababu kuna kila kitu darasani, kuna zana za kufundishia, wakati mwingine wanajifunza kupitia televisheni na au tunawawekea projector.”

Macha anaongeza:”kwa vitu hivyo vinamfanya mwanafunzi kuwa rahisi kwakwe kujifunza hata mwalimu pia inakuwa ni rahisi kufundisha, hutumii nguvu nyingi.”

Mmoja wa wazazi wa mwanafunzi katika shule ya Mikongani, Tatu Nyamoga alishukuru Serikali ya Rais Samia Suluhu Hassan kwa kuendelea kuboresha sekta ya elimu.

“Wazazi wengi wanatamani watoto wao wasome katika shule nzuri lakini vipato vyetu ni kidogo kwani shule binafsi gharama ni kubwa na wakati mwingine hata mazingira si mazuri unalazimika kumpeleka kwa hiyo. Kwa hiyo ujio wa shule hii na madarasa katika eneo letu kwetu ni ukombozi mkubwa.”

Mwalimu Mkuu wa Shule ya Msingi Mikongeni, Saimon Mndendemi anasema shule imepokea Sh milioni 55.824 ujenzi wa madarasa ya awali ya mfano.

“Awali tulikuwa na madarasa kwa wanafunzi wa awali lakini hayakuwa na kiwango bora kama ilivyo sasa na yalikuwa wanafanya tupokee wanafunzi wachache lakini sasa idadi ya wanafunzi imeongezeka kutoka wanafunzi 60 mpaka wanafunzi 135 ambao wanasoma kwenye madarasa ya awali ya mfano.”

“Kwa kweli ni madarasa ya kipekee ambayo yanamfanya mtoto atake kuwapo shuleni muda wote na pindi wazazi wao wanawafuata kuwachukua wanalia na kutotamani kuondoka hii ni kutokana kuwa na madarasa mazuri na mazingira mazuri ya kufundishia na kujifunzia.”








SERIKALI kwa kushirikiana na wadau wa maendeleo imelenga kuongeza fursa ya upatikanaji na ushiriki katika elimu bora kwa watoto wote nchini kuanzia ngazi ya elimu ya awali, msingi na nje ya mfumo rasmi hususan wanaotoka katika mazingira hatarishi.

Katika kutimiza hilo, Serikali kupitia Wizara zenye dhamana ya kusimamia Sekta ya Elimu ambazo ni Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, na Ofisi ya Rais-Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa wametekeleza Mradi wa Kuimarisha Stadi za Kusoma, Kuandika na Kuhesabu Awamu ya Pili (GPE – LANES II).

Utekelezaji wa mradi huo pamoja na mambo mengine pia umegusa watoto wenye mahitaji maalum. Mradi umewezesha ufanyikaji wa zoezi la ubainishaji wa Watoto wenye mahitaji maalum katika kata 3,785 kati ya 3,956 sawa na asilimia 95.7. Katika zoezi hilo watoto waliojitokeza walikuwa 59,784 kati yao watoto waliobainishwa kuwa na mahitaji maalum walikuwa watoto 28,690 na walitakiwa kuandikishwa shuleni.

Pia umewezesha ununuzi wa vifaa visaidizi mbalimbali kwa ajili ya wanafunzi wenye mahitaji maalum katika mikoa 26 ya Tanzania Bara sambamba na kujenga hosteli 20 za wanafunzi wenye mahitaji maalum.

Mkurugenzi Msaidizi wa Elimu ya Awali na Msingi, Ofisi ya Rais TAMISEMI Suzan Nyarumba Nusu anasema kupitia Mradi wa GPE LANES II kumefanyika uboreshaji katika vituo mbalimbali ambavyo vinatoa elimu maalum kwa watoto wetu wenye mahitaji maalum ambapo vituo 13 vimefanyiwa ukarabati na ujenzi wa miundombinu.

Anasema kupitia mradi huo pia vifaa visaidizi vinavyogharimu takribani Sh bilioni 1.2 vimepelekwa kwenye shule kwa ajili ya kuwasaidia watoto wenye mahitaji maalum ambao wako katika shule zetu mbalimbali nchini.

"Kwa hiyo kujifunza kwao imekuwa rahisi na imeturahisishia pia sisi walimu katika kufanya kazi, tunaishukuru sana serikali bila kumsahau Rais Samia kwa kuwakumbuka watoto wetu wenye mahitaji maalum."

Kwa Kanda ya Ziwa mkoani Geita, GPE LANES II haijawacha ukiwa bali imeacha tabasamu ambapo Mwalimu Mkuu wa Shule ya Msingu Mbugani Manispaa ya Geita, Edwik Ndunguru anasema huu mradi umeweza kuboresha miundombinu ya shule yake ambayo ni shule jumuishi.

"Mwaka 2020 Serikali ilituwezesha na tukapokea Sh milioni 40 kwa ajili ya mradi wa kukuza stadi za kusoma, kundika na kuhesabu, fedha hizo zimetuwezesha kujenga vyumba viwili vya madarasa, ambayo vinavyotumiwa na wanafunzi wa darasa la kwanza na la pili."

Kwa upande wa elimu maalum katika Shule ya Msingi Mbugani, Sista Adela Temba mwalimu wa kitengo cha elimu maalum katika shule hiyo anasema tunaishukuru serikali kwa maana imetujengea mabweni pamoja na madarasa.

"Watoto wenye mahitaji maalum walikuwa wanapata sana changamoto mtaani hasa walemavu wa ngozi ambao mara nyingi walikuwa wanajeruhiwa kutokana na imani potofu lakini hao wote wako hapa wakiwa salama."

Mwalimu wa Shule ya Msingi Tumaini Viziwi iliyopo Manispaa ya Singida, Rosemary Kiwale anasema mafunzo endelevu kazini yamekuwa na msaada sana katika kutatua changamoto za kielimu kwa watoto wenye mahitaji maalum.

"Mfano katika darasa langu la kwanza la wanafunzi wenye mahitaji maalum utakuta kuna mahiri ambazo ni ngumu kwa watoto wa darasa la kwanza kwa mfano mbinu ya kusoma kwa ufasaha."

"Hivyo naenda kwa walimu wenzangu naomba wanisaidie, tunakaa tunajadiliana na nikirudi darasani nakuwa confortable (nakuwa huru) kwasababu natumia njia ambazo walimu wenzangu wamenisaidia nawasaidia watoto wangu."

Mwalimu Shule ya Msingi Tumaini Viziwi, Frances Edward anasema mradi wa GPE LANES II umewanufaisha kwa upande wa vifaa na kupunguza watu wasiojua kusoma, kuandika na kuhesabu kwa wanafunzi wenye mahitaji maalum.

"Mradi huu umetunufaisha kwenye eneo la vifaa vya kupimia watoto, shule zote za wanafunzi viziwi zinatakiwa kuwa na vifaa kwa ajili ya upimaji na ufundishaji namna ya kuongea."

"Hivyo mradi wa GPE LANES II umetusaidia kupata mshine za upimaji ambazo zinatumika kwa ajili ya kuwapima watoto wetu kuangalia viwango vyao vya usikivu na pia kuwasaidia kusoma na kutamka maneno."

Anasema kupitia mradi huo kiwango cha wasiojua stadi za kusoma, kuandika na kuhesabu kwa wanafunzi wa darasa la kwanza, la pili na awali kimepungua.

Mwalimu wa Tumaini Viziwi, Alfred Baganda anasema vifaa visaidizi ambavyo shule imevipokea zinawasaidia wanafunzi kujifunza zaidi kwa vitendo kuliko nadharia kwa hiyo wanajifunza vitu vingi ambavyo vinasaidia kuwaongezea ujuzi na stadi za maisha.

"Tuna mfano mzuri mwanafunzi ambaye ametoka Shule ya Msingi Tumaini Viziwi ambaye kwa sasa anafanyakazi ya kushona viatu mtaani, vifaa hivi vikitumika vizuri



# Wanafunzi wenye mahitaji maalum walivyoguswa na mradi wa GPE



vitasaidia wanafunzi wakuongeza ujuzi na stadi za maisha."

Mwalimu Sara Makage wa Shule ya Msingi Kalolieni wa Halmashauri ya Jiji la Arusha anaishukuru Serikali kwa kujali wanafunzi wenye walemavu wa akili.

"Tumefaidika kuletewa vifaa hivi ambavyo vimekuwa na manufaa sana kwa watoto wetu pia vinawachangamsha hasa kwa watoto wenye matatizo ya viungo vya mikono."

"Pindi wanapotumia zile zana wanajitahidi kushika zile zana na zinampa mazoezi ya vidole na mikono yake pia."

Mwalimu Mkuu wa Shule ya Msingi Kibaoni katika Halmashauri ya Wilaya ya Chunya, Gloria Njelwa anasema wamepokea Sh milioni 100 kwa ajili ya ujenzi wa bweni na wanafunzi wenye mahitaji maalum.

"Kwa Wilaya ya Chunya hatukuwa na shule yotote ambayo ina mabweni kwa ajili ya watoto wetu wenye mahitaji maalum."

Mzazi wa mwanafunzi katika shule ya msingi Kaloleni anasema: "nitoe shukrani kwa Rais kwani mradi huu umekuwa na manufaa kwa watoto wetu kwa kuwajengea madarasa, kutoa chakula cha mchana na bweni na sasa watoto wengi wametoka ndani na wamekuja shule."

Kaimu Mkurugenzi Elimu Maalum na Michezo ofisi ya Rais TAMISEMI Godliver Nkala alitoa wito kwa jamii ya watanzania ambao wana watoto wenye ulemavu wa aina yoyote wasiwafiche.

"Wazazi msiwafiche watoto wenye mahitaji maalum kwa sababu wataalamu tunao, fursa zipo. Tulichokibaini watoto hawa wanavipaji na uwezo wa kujifunza wanafundishika na wanauwezo wa kuchangia katika nguvukazi ya taifa."

Anasema Ofisi ya Rais-TAMISEMI imeendelea kutoka msukumu kwa wakuu wa mikoa, wilaya na wakurugenzi kuwathamani watoto wenye mahitaji maalum ili wapate elimu kama watoto wengine.

> **Kwa hiyo kujifunza kwao imekuwa rahisi na imeturahisishia pia sisi walimu katika kufanya kazi, tunaishukuru sana serikali bila kumsahau Rais Samia kwa kuwakumbuka watoto wetu wenye mahitaji maalum.**



# Programu ya GPE

## Ilivyoondoa changamoto kwa Taasisi za Umma, Shule za Msingi

ELIMU ni uwekezaji muhimu ambao nchi yoyote Duniani inafanya ili kusaidia watu wake kuwa na ujuzi wa aina mbalimbali ili waweze kufanya kazi kukuza uchumi wa nchi yao lakini pia kuibua fursa mbalimbali kwa wananchi na wawekezaji katika Sekta zote.

Prof. Adolf Mkenda Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia anasema kupitia Programu mbalimbali Serikali imeongeza na kuboresha miundombinu ya shule zake kuanzia miundombinu ya awali mpaka vyuo vikuu kwa mfano kwenye shule za msingi Mradi wa GPE LANES II umewezesha ujenzi wa vyumba vya madarasa, matundu ya vyoo, Vituo vya walimu, mabweni ya wanafunzi wenye mahitaji maalum, madarasa ya awali ya mfano na nyumba za walimu ambayo yamejengwa kote nchini.


Prof. Mkenda anaongeza kuwa Serikali inasisitiza kutoa elimu jumuishi ambayo haibagui mtoto yeyote kwani hata watoto wenye mahitaji maalum kwa hivi sasa wanasoma katika mazingira bora kulingana na maumbile yao bila kutengwa.

“ni imani yetu kwamba elimu ni haki ya kila mtu, kila mtoto lazima apate fursa ya kupata elimu, Tanzania inatoa msisitizo wa usawa katika elimu, Serikali inaendelea kuhakikisha elimu tunayoitoa ni jumuishi, watoto wenye mahitaji maalum wanasoma bila kutengwa” anasema Prof Mkenda.

Kuhusu Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA), Prof Mkenda anasema usambazaji wa vifaa vya TEHAMA katika shule na Taasisi nchini ni utekelezaji kwa vitendo na dhamira ya Serikali inayoongozwa na Dkt. Samia Suluhu Hassan Rais wa Jamhuri ya Muungano ambaye amesisitiza matumizi ya TEHAMA ili kuchochea uchumi na kuendana na kasi ya mabadiliko ya Sayansi na Teknolojia hususani Sekta ya Elimu.

Kuhusu wanafunzi wenye mahitaji maalum, Prof. Mkenda anasema mpaka sasa Serikali imeshatumia Shilingi Bilioni 4.5 kwa ajili ya ununuzi wa vifaa vya kufundishia na kujifunzia kwa ajili ya wanafunzi wenye mahitaji maalum na kwamba kwa wanafunzi wenye changamoto kubwa Serikali imeongeza shule ya sekondari Patandi iliyopo mkoani Arusha na shule ya msingi Lukuledi iliyopo Masasi mkoani Mtwara ili kukuondoa changamoto za miundombinu na kuhakikisha watoto wenye mahitaji maalum wanapata elimu bila kikwazo.

Prof. Carolyne Nombo Katibu Mkuu Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia anasema Serikali kwa kushirikiana na Wadau wa GPE walitoa Shilingi Bilioni 243 kwa ajili ya kuboresha Stadi za Kusoma, Kuandika na Kuhesabu (KKK) lakini pia shughuli mbalimbali zinaendelea katika mikoa yote kama ujenzi wa miundombinu ya shule za awali 128 za mfano na marajio kama Serikali ni kuona mfano wa shule hizo





(model) inafuatwa lakini pia Mradi ulijenga shule 17 kusaidia wanafunzi wenye mahitaji maalum zinazozingatia mahitaji halisi ya wanafunzi hao.

Mradi wa GPE pia umeboresha masuala ya uthibiti ubora kwani elimu bila ubora haiwezi kwenda, Wathibiti Ubora waliandaa matini mbalimbali katika kazi zao na kuwezesha mafunzo kwa viongozi wa kielimu kurahisisha ufuatiliaji katika shule.

Mradi pia umesaidia kufanya ukarabati na kuboresha Vituo vya Walimu (TRC) 308 ili walimu wa shuleni waweze kuvitumia karibu na maeneo yao pia wametoa moduli (Mwongozo) ambazo zinatumiwa kwenye Vituo vya Walimu (TRC) kufanya mafunzo na tathmini ya vituo hivyo.

Prof. Nombo amewashukuru Watekelezaji waliopo kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa usimamizi mzuri, shukrani za pekee kwa Wadau wa Maendeleo GPE na Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. Samia Suluhu Hassan

Hasheem Dafa Mwalimu Mkuu shule ya Msingi Mruazi Halmashauri ya Wilaya ya Korogwe mkoani Tanga anasema tangu shule hiyo kuanzishwa mwaka 1972 chini ya umiliki wa Mamlaka ya Mkonge shule hiyo ilikuwa chakavu sana na miundombinu haivutii na ndipo GPE walisikia kilio chao na kupatiwa Shilingi milioni 400 ambapo walijenga madarasa 14 na kuweka samani pamoja na ujenzi wa nyumba mbili za walimu mbili kwa moja ambazo zimeondoa changamoto ya makazi kwa baadhi ya walimu.

Mafanikio ya shule ya msingi Mruazi yanathibitishwa na mwanafunzi Khamis Nduhuru anasema "mwanzoni nilikuwa nasoma shule ya msingi Mluzi ambayo ilikuwa mbali na nyumbani, na mazingira yake yalikuwa ni porini, ukitembea unakuwa una wasiwasi, na muda wa kujisomea hakuna, unaweza tembea hadi saa moja kufika nyumbani,



na muda wa kusoma hakuna, lakini sasa ni karibu, mazingira mazuri, muda wa kusoma upo, asante Mheshimiwa Rais mama Samia Suluhu" anasema Khamis Nduhuru.

Angela Kitali Mkurugenzi Baraza la Mitihani Tanzania (NECTA) anasema Mradi umewezesha kufanya uendeshaji wa upimaji kitaifa wa Stadi za Kusoma, Kuandika na Kuhesabu (KKK) lakini pia kuandaa, kuchapa na kusambaza vitabu vya upimaji darasa la nne kuonyesha namna ulivyofanyika pamoja na mtihani wa kumaliza elimu ya msingi (darasa la saba) na vitabu hivi vya upimaji vimewasaidia walimu kuona wanafunzi walivyojibu maswali na kung'amua ugumu uliokuwepo kwa baadhi ya maswali ili waweze kuboresha na kazi nyingine ni kufanya mafunzo kwa walimu 3,576 wenye umahiri wa kufundisha darasa la kwanza na la pili namna bora ya kupima wanafunzi katika ngazi hii.

Dkt. Anitta Komba Mkurugenzi wa Taasisi ya Elimu Tanzania (TET) anasema Taasisi yake iliwezeshwa Shilingi Bilioni 62 na Programu ya GPE LANES II katika kufanikisha uandaaji na uchapaji wa moduli na hivyo kuondoa changamoto ya vitabu vya kiada kwa wanafunzi.

"kupitia Mradi wa GPE LANES II tulipokea 67,218,310,919 kwa ajili ya kuchapa vitabu vya kiada vya awali hadi darasa la saba, uwiano kutoka awali hadi darasa la tano vitabu 2 kwa mwanafunzi mmoja, darasa la sita hadi darasa la saba kitabu kimoja kwa mwanafunzi mmoja" anasema Dkt. Komba.

Pia vitabu vya wanafunzi wenye mahitaji maalum vilibadilishwa na kuwekwa katika mfumo wa breille na michoro miguso vitabu vyote vimebadilishwa, vikachapwa na kusambazwa hapa uwiano upo kwa vitabu 3 kwa mwanafunzi mmoja (breille) na vitabu vyenye maandishi makubwa kwa uwiano wa kitabu kimoja kwa mwanafunzi mmoja na hii ni kwa ajili ya wanafunzi wenye uoni hafifu. Katika Taasisi hiyo kuna studio ya kisasa ya kurekodi sauti GPE iliunga mkono kwa kutoa fedha za kununua vifaa vya kurekodia sauti.





# GPE ilivyoongeza umahiri walimu, wawa kidigitali

KATIKA kuimarisha ubora wa ufundishaji na ujifunzaji program ya GPE-LANES pia imewezesha Mafunzo Endelevu ya Walimu Kazini (MEWAKA) kwa kuwajengea uwezo walimu wa elimu ya awali, msingi, elimu maalum na wakufunzi wa MEMKWA.

Mafunzo hayo yamewafikia wawezeshaji wa kitaifa 195, viongozi wa elimu 984 na walimu mahiri wa elimu ya awali na msingi 30,550.

Pia imewezesha ununuzi wa vifaa vya TEHAMA ikiwa ni pamoja na kompyuta za mezani 600, projekta 150, printa 150 na mashine za kudurufu 150 kwa ajili ya vituo vya walimu 150 vilivyoko kwenye halmashauri 144 kwa awamu ya kwanza.

Kwa awamu ya pili zimenunuliwa kompyuta za mezani 640, projectea 160, printer 160 na mashine za kudurufu 160 kwa ajili ya vituo vya walimu 309.

Mkurugenzi Msaidizi wa Elimu ya Awali na Msingi, Ofisi ya Rais-TAMISEMI, Suzan Nyarubamba Nussu anasema kupitia mradi wa GPE LANES II wamewezesha walimu kupata sehemu nzuri ya kubadilishana umahiri.

"Tumeweza kujenga na kufanyia ukarabati vituo vya walimu lakini pia kununua vifaa kama kompyuta ili mazingira yawe tulivu na yanayowawezesha walimu kukaa kwa utulivu na kujifunza vizuri na kubadilisha uzoefu wa maarifa ya ufundishaji."

"Tunaishukuru Serikali ya Rais Samia Suluhu Hassan kwa jinsi inavyoendelea kuwekeza katika sekta ya elimu kwa lengo la kuwasaidia walimu kuboresha utaalamu wao."

Afisa Taalum Manispaa ya Morogoro, Amani Mfaume anasema mafunzo ya MEWAKA yameongezea umahiri kwa walimu na kuendelea kuzifahamu mada zilizokuwa changamoto kwao, hivyo kuwa na matokea makubwa na mazuri kwa watoto.

Mratibu wa Mafunzo Endelevu ya Walimu Kazini Morogoro, Rhoda Sheba anasema kupitia program ya GPE-LANES II vituo vya walimu vimeboreshwa na kuwekewa vifaa vya kisasa ambavyo vimesaidia walimu kujifunza kwa njia ya kidigitali.

Rajab Mpela mwalimu shule ya msingi Kikundi

> **Tunaishukuru Serikali ya Rais Samia Suluhu Hassan kwa jinsi inavyoendelea kuwekeza katika sekta ya elimu kwa lengo la kuwasaidia walimu kuboresha utaalamu wao.**







mkoani Morogoro anasema vifaa vya TEHAMA vilivyowekwa kwenye vituo vya mafunzo vimesaidia ujifunzaji kwa njia ya vitendo.

Anasema vimesaidia walimu kuwa mahiri kwenye program mbalimbali kama program andishi na program jedwali (exel) ambazo zinamchango katika shughuli za kila siku za walimu.

“Kabla ya maboresho ilikuwa ngumu kufundishana mada zinazohusiana na TEHAMA na matumizi ya Kompyuta kwa walimu kwasababu tulikuwa tunasoma kwa nadharia kwa kuandikiana ubaoni.”

“Mfano unapomfundisha mwalimu program jedwali (exel) katika kupanga matokeo ya wanafunzi ililazimu kufundisha kwa kuandika na kuchora ubaoni kitu ambacho kilikuwa kigumu kwa walimu kuelewa matumizi sahihi ya program.”

Mwalimu wa Shule ya Msingi Konga, Gabriel Peter anasema mafunzo yamemsaidia ujuzi zaidi ikiwamo kupata mbinu mpya na hatua sahihi za kuwafundisha watoto wa dogo ili waelewe kwa Lugha ya Kiingereza.

Mwalimu Mkuu wa Shule ya Msingi Ukombozi, iliyopo Manispaa ya Singida, Yesaya Samweli anasema:”mafunzo yamesaidia wanafunzi wetu kupokea elimu na maarifa yanayostahili na kumuelewa vizuri mwalimu.

“Tumekuwa tukifundishana jinsi ya kuenenda na mada tata ambazo zinamfanya mwalimu ashindwe kufundisha vizuri na kushindwa kujiamini.”

“Kwa program hii walimu wamekuwa mahiri na idadi ya wanafunzi hawajamudu stadi za kusoma, kuandika na kuhesabu ni kidogo sana na tunaamni ndani ya muda mfupi wote watakuwa wanamudu stadi za KKK.”

Mratibu wa MEWAKA Ngara Mjini mkoani Kagera, Emmanuel Bubelwa anasema vifaa vya TEHAMA vimerahisha mafunzo kwa walimu na kutoa matokeo chanya.

“Kwa sasa hatuna tena mfumo wa kutoa mtihani kwa kuandika ubaoni, wanafunzi wetu wamehama kwenye kufanya mtihani uliondikwa ubaoni kwa kufanya uliochapwa na ni kwa madarasa yote.”

“Walimu wanakuwa wepesi kufanya kazi zao na hata mitihani ya mwisho wanafunzi wanafanya vizuri kwasababu wanakuwa na uzoefu wa kuona mitihani kwenye karatasi.”

Mwalimu Mkuu Shule ya Msingi Tumaini Viziwi iliyopo manispaa ya Singida, Francess Edward anaishauri serikali kuongeza wigo wa program ya MEWAKA iwe endelevu na kuwafikia walimu wengi zaidi ili kuwaondoa walimu kufundisha kizamani na kwenda na wakati.

“Tunaishukuru serikali kwani program hii imekuwa na tija, tunaomba wigo uongezwe kwani walimu wanahitaji mafunzo ili wafanyekazi kwa ufanisi, dunia inaenda inabadirika na mwalimu wanapaswa wabadirike kama dunia inavyobadilika.”






# Wadau wafurahishwa na utekelezaji wa mradi wa GPE

WADAU wa Maendeleo wanaosaidia kuendeleza elimu ya msingi nchini kupitia mradi wa GPE wameonesha kufurahishwa na utekelezaji wa mradi huo ambao unaelekea ukingoni.

Akizungumza wakati wa ziara ya ukaguzi wa utekelezaji wa miradi hiyo, Msimamizi wa Ufadhili kwa Serikali ya Tanzania, Ubalozi wa Sweden, Tanzania Stella Mayenje anasema ameridhishwa na kazi iliyofanyika hatua ambayo imemtia moyo.

"Nimeridhishwa kwa kuoana kazi hii, kitu ambacho kimenitia moyo sana, nikuona jinsi ambavyo kamati za shule zimekuwa zinawajibika kwenye kusimamia utekelezaji wa mradi huu."

"Lakini kitu cha pili ambacho nimekibaini tangu tumeanza ziara ni haya madarasa (madarasa ya mfano) yamechukuwa watoto wengi sana lakini nikajaribu kufanya tathimini na kwenda mbele zaidi nikaangalia darasa la pili unakuta wanafunzi wako wachache."

Mayenje anaongeza: "kwa maana hiyo haya madarasa ya mfano yamewavutia wazazi kuleta watoto kwasababu wanaona wako mahali salama, kuna walimu, wanafunzishwa vizuri kuna sehemu ya watoto kucheza na nimeona ni kitu kizuri sana kwa hiyo nimetiwa moyo sana."

Pia anatumia fursa hiyo kuipongeza Serikali kwa kusimamia

> **Tumefika tumejionea madarasa mazuri, nimeyapenda haya madarasa, na najivunia GPE pia imechangia pia na hii ni njia nzuri ya kutumia rasilimali fedha zinazotolewa kwa ajili ya kusaidia ujenzi wa madara ya awali kama haya.**

kwa umakini fedha za mradi hiyo ambayo imeendana na thamani ya fedha.

"Kwa bajeti yetu tulipanga kujenga madarasa 300 lakini kinachoonekana yatajengwa madarasa 436 kwa bajeti ile ile kwa hiyo ni kitu kizuri sana kwasababu wameweza kuangalia thamani ya fedha na mchango wa jamii imefanya kitu kikubwa sana napenda kuwapongeza sana."

Naye Msimamizi wa Ufadhili kwa Serikali ya Tanzania Ubalozi wa Sweden, Tanzania,

Alexandro Lian anasema wadau wa maendeleo wamekuwa matari wa mbele kusaidia semta ya elimu nchini kupitia miradi ya Lipa kulingana na Matokeo(EP4R) na mradi wa GPE LANES.

"Ninasikia fahari kwa ushirikiano na serikali ya Tanzania katika sekta ya elimu na tumekuwa tukisaidia sekta ya elimu ya Tanzania kupitia mradi wa EP4R lakini pia GPE kwa miaka sita tuliyoanza ushirikiano na Tanzania."

"Tumefika tumejionea madarasa mazuri, nimeyapenda haya madarasa, na najivunia GPE pia imechangia pia na hii ni njia nzuri ya kutumia rasilimali fedha zinazotolewa kwa ajili ya kusaidia ujenzi wa madara ya awali kama haya."

"Niwatakie kila la kheri na nimatumaini yangu kuwa ushirikiano wetu utaendelea kwa siku za usoni."

Mradi huo unatekelezwa kwa ufadhili na ushirika wa kimataifa wa kusaidia maendeleo ya elimu (GPE) kwa msaada wa Sh bilioni 264.6 ukilenga kuongeza fursa ya upatikanaji na ushiriki katika elimu bora kwa watoto wote nchini kwa ngazi ya elimu ya awali, msingi na elimu ya nje ya mfumo rasmi hususani wanaotoka katika mazingira hatarishi na wenye uhitaji mkubwa wa fursa ya elimu ya msingi.










# Serikali na Wadau Kufanikisha Mafanikio ya Elimu nchini Kupitia Programu ya GPE

Taasisi ya GPE iliundwa mwaka 2002 kwa lengo la kusaidia nchi zinazoendelea kuimarisha mifumo ya elimu. GPE kwa sasa inahudumia nchi washirika zaidi ya 80 ulimwenguni, na Tanzania ni mojawapo ya washirika tangu mwaka 2013. GPE ni mfuko mkubwa zaidi wa kimataifa unaojihusisha na masuala ya elimu, na lengo lake kuu ni kuimarisha mifumo ya elimu katika nchi zenye kipato cha chini. Mpango mkakati wa GPE unazingatia kuboresha ujifunzaji, usawa, na ujumuishi ili kuhakikisha kwamba watoto wote walio katika umri wa kwenda shule wanapata fursa bila kuacha mtoto yeyote nyuma.

Rais Mstaafu wa Awamu ya Nne wa Tanzania Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete ambaye ni Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi wa Taasisi ya Ushirikiano wa Elimu Duniani (Global Partnership for Education) na mwafrika wa kwanza kushika wadhifa huo, alikuwa Mgeni rasmi katika Hafla ya Kutambua Mchango wa Wadau katika Sekta ya Elimu, hafla iliyofanyika tarehe 30 mwezi Agosti, 2023 Jijini Dar es Salaam na kuhudhuriwa na Wakuu wa Mikoa  na Wadau wa Elimu kutoka mikoa yote ya Tanzania Bara wakiwemo Wadau wa Elimu kutoka nje ya nchi.

Aidha, Wadau hao kutoka kwenye mikoa ya Tanzania Bara kwa nyakati tofauti walishawishiwa na Serikali kuchangia kuweza kuchangia fedha taslimu au kufanya ujenzi wa miundombinu ya elimu kwenye shule za msingi kama sehemu ya kuiunga mkono Serikali kuboresha elimu na kufikia kwa haraka malengo ya milenia ambayo yanasisitiza elimu bora, yenye usawa na inayotolewa kwa watoto wote.









> mkutano wa Wahisani hao wa Taasisi ya GPE unatarajiwa kufanyika nchini Tanzania Visiwani Zanzibar mapema mwakani na itakuwa ni mara ya kwanza kwa Tanzania kuwa mwenyeji lakini pia mara ya kwanza kufanyika katika ardhi ya Bara la Afrika.





Hafla hiyo ya kihistoria iliwaleta Wadau wa ndani na nje ya nchi pamoja ili kuchangia kwenye Sekta ya Elimu kwa ajili ya kupata fedha za ruzuku kutoka kwa Wadau GPE kama motisha lakini pia katika kuijengea uwezo Serikali kuwaunganisha Wadau kuchangia Sekta ya elimu ambapo Taasisi ya GPE inatoa mchango wa dola moja kwa kila dola moja iliyochangiwa na Wadau hao.

Dkt. Kikwete anasema kuwa mkutano wa Wahisani hao wa Taasisi ya GPE unatarajiwa kufanyika nchini Tanzania Visiwani Zanziba mapema mwakani na itakuwa ni mara ya kwanza kwa Tanzania kuwa mwenyeji lakini pia mara ya kwanza kufanyika katika ardhi ya Bara la Afrika.

Aidha, ili upate fedha za ruzuku za GPE ni pale unaposamehewa mkopo kwa ahadi ya msamaha huo ili fedha hiyo ambayo mngeilipa kama deni mnaipeleka kwenye elimu, hapo kila dola tatu GPE pia inachangia dola tatu kwa kila dola moja iliyosamehewa. Hali hii pia ni jitihada binafsi kama nchi kuongea na nchi zinazowadai madeni ili kupata fedha zaidi kuboresha elimu.

Dkt. Kikwete pia amefafanua kwa kusema mfano mzuri pia ni wakati wa kipindi cha COVID-19, Mfuko wa GPE ulitoa msaada wa Dola milioni 500 kwa nchi 66 na Tanzania ilinufaika kwa kupatiwa dola

Inaendelea uk 22




Inatoka uk 21

milioni 15 ili kuwawezesha watoto kusoma katika kipindi cha COVID-19 ambapo manufaa ndiyo yale yote ya kuimarishwa miundombinu ya elimu na pia eneo la la ufundishaji na ujifunzaji wa wanafunzi na walimu nchini.

Dkt. Kikwete alipongeza utaratibu wa kukutana kama ulivyofanyika kunatoa fursa nzuri kwa Wadau wote kushirikiana na Serikali ili kuendeleza sekta ya elimu yenye umuhimu mkubwa nchini na ndio maana mataifa karibu yote Duniani yanaendeshwa na Sayansi kwa kuzingatia hilo na kupia kipaumbele sayansi nchi inapaswa kuweka mazingira wezeshi yatakayoondoa changamoto zinazosababisha wanafunzi kufeli masomo ya sayansi na mikakati yetu ibaki kwa kuwawezesha wanafunzi kusoma masomo ya Sayansi ili waje kusaidia uchumi wa nchi.

"Kutokana na hali hii tunapaswa kuandaa mkakati wa kujadili na kuelezea changamoto zinazosababisha wanafunzi wafeli ili kuweka mikakati yetu sawa kazi ibaki kwa wanafunzi" alisema Dkt. Kikwete.

Hivyo basi, katika kuhakikisha nchi inafikia lengo la kupata fedha kwa kipengere cha GPE multiplier, Dkt. Kikwete ametoa wito kwa Wakuu wa Mikoa wote walioahidi kutoa fedha ambazo ni zaidi ya Shilingi Bilioni 465 kama ahadi ambazo zitaisaidia nchi kupata fedha za ruzuku (grant) kiasi cha Dola milioni 50.

"tumeshasikia jinsi ahadi zilivyotolewa, zaidi ya shilingi Bilioni 465, matumaini yangu walioahidi watatoa, ahadi ni deni, Wakuu wa Mikoa mmetoa ahadi wenyewe hapa" alisema Mheshimiwa Dkt. Jakaya Kikwete.

Aidha, Kikwete amesema miradi ya GPE nchini, ilifadhiliwa kwa awamu mbili ambazo ni za mwaka 2014 hadi 2018, na 2018 hadi 2023 ikihusisha ujenzi wa madarasa mapya ya shule za msingi 2,980, mabweni ya wanafunzi wenye mahitaji maalum 14, matundu ya vyoo 7,673, shule mpya 18, nyumba za walimu 94, ukarabati wa vituo vya walimu 13 (TRC), ujenzi na uendeshaji wa vituo vya walimu 12, uendeshaji wa Mafunzo ya Walimu Kazini (MEWAKA) na ununuzi wa vifaa vya Kufundishia na Kujifunzia kwa walimu na wanafunzi.

Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Mheshimiwa Prof. Adolf Mkenda alisema Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan amejenga imani kubwa kwa Sekta Binafsi nchini na ndio maana Wadau wameitikia kwa kiwango kikubwa na kuendelea kutoa michango yao kwenye elimu hapa nchini na hivyo ni jambo jema kwa wizara ya Elimu na Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) kutambua mchango wa Wadau kwenye Sekta ya Elimu nchini.

Prof. Adolf Mkenda aliongeza kuwa kutambua mchango wa wadau kwenye Sekta ya elimu ni kuendelea kuhimiza Sekta binafsi na wadau kushirikiana na Serikali ili kufanikisha utoaji wa elimu bora nchini pamoja na mageuzi ya elimu kwani kuwekeza kwenye elimu ni nyenzo muhimu ya kusaidia nchi kwenda mbele na kwamba tofauti ya maendeleo ya nchi duniani haitokani na kuwa na mafuta, madini na rasilimali za asili bali inatokana zaidi na watu wake kuelimika na kuweza kutumia

> **Kutokana na hali hii tunapaswa kuandaa mkakati wa kujadili na kuelezea changamoto zinazosababisha wanafunzi wafeli ili kuweka mikakati yetu sawa kazi ibaki kwa wanafunzi**



sayansi na teknolojia katika sekta zote.

"Hakuna namna ya kukwepa kuwekeza kwenye elimu na kuwekeza kwenye elimu ni kuwekeza kwa vizazi na vizazi, kwa hiyo Rais wetu alivyoongeza fedha kwenye elimu haangalii uchaguzi ujao, anaangalia kizazi kijacho,"alisema Prof. Mkenda.

Kuhusu maboresho yanayoendelea kwenye Sera ya elimu nchini alisema kuwa Sera hiyo ipo kwenye mchakato wa kuipeleka Bungeni na mapendekezo yake yatafanyika katika mwezi Septemba, 2023 kabla ya kutangazwa kuanza kutumika lengo kubwa likiwa ni kuboresha, kuchangia Sekta ya elimu ili kuifanya kuwa Bora zaidi na yenye tija kwa maslahi ya nchi kwani kuendeleza elimu kuna gharama kubwa ikiwa ni pamoja na maoni na michango mbaliimbali ya Wadau.

"Sera ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi ya mwaka 2014 tuliangalia mambo ya msingi ambayo yamewekwa haya-jafanyiwa kazi ikiwemo elimu ya msingi itakuwa miaka sita na minne sekondari jumla kumi (mtoto) anamaliza shule akiwa na miaka kumi na sita" alisema Prof. Mkenda.

Katibu Mkuu Ofisi ya Rais TAMISEMI Adolf Ndunguru alitoa rai kwa Wakuu wa Mikoa kuweka utaratibu mzuri wa usimamizi wa utekelezaji wa ahadi zilizowekwa na Wadau, kuanzisha 'Kanzidata' kwa kila mkoa ili kurahisisha ufuatiliaji na tathmini ya ahadi zilizotolewa lakini pia kuendelea kuwaelimisha Wadau kwa kuwa zoezi hilo la kuiunga mkono Serikali kuboresha elimu nchini ni endelevu.

Ahadi za fedha zilizotolewa kutoka kwenye mikoa yote ya Tanzania Bara mpaka siku ya hafla ya Wadau wa Elimu nchini zilikuwa ni Shilingi Bilioni 465,686,988,538.86 ambapo mkoa wa Mara (Bilioni 155,010,019,742.38), Arusha (1,835,300,000.00), Dar es Salaam (Bilioni 9,373,253,787.90), Dodoma (Bilioni 14,587,330,22454), Geita (Bilioni 10,700,000,000.00), Iringa (Bilioni 5,511,543,750.00), Kagera (Bilioni 6,303,191,952.86), Katavi (Bilioni 24,901,824,096.00), Kigoma (Bilioni 1,002,409,068.00), Kilimanjaro (Bilioni 6,285,555,105.00), Lindi (Bilioni 4,642,676,692.00), Manyara (Bilioni 13,709,622,456.00), Mbeya (Bilioni 4,435,052,000.00), Morogoro (Bilioni 1,883,096,000.00), Mtwara (Bilioni ,2253,500,000.00), Mwanza (Bilioni 9,244,955,523.48), Njombe (Bilioni 7,800,970,737.12), Pwani (Bilioni 55,818,074.12), Rukwa (Bilioni 4,136,197,110.50), Ruvuma (Bilioni 4,942,891,000.00), Singida (Bilioni 88,273,435,148.94), Simiyu (Bilioni 1,903,689,480.00), Shinyanga (Bilioni 1,235,254,800.00), Songwe (Bilioni 8,993,057,483.02), Tabora (Bilioni 2,109,855,000.00) na Tanga (Bilioni 14,793,862,761.00).

Mpaka sasa Washirika wa GPE Duniani wametoa msaada wa kifedha kwa nchi 88 ili kuinua Sekta ya elimu na kutimiza lengo la kutomuacha nyuma mtoto yeyote katika kupata haki ya elimu.

Kuhusiana na ahadi zilizotolewa na Wadau Mhe. Kikwete alisema: "naomba msije mkanitia aibu, naomba ahadi hizi zitimizwe, nitahitaji nione utekelezaji ifikapo wakati wa mkutano mkuu wa mwaka wa GPE utakaofanyika Zanzibar mapema mwakani, 2024. Itakuwa ni mara ya kwanza kwa Tanzania kuwa mwenyeji lakini pia mara ya kwanza kufanyika katika ardhi ya Bara la Afrika.





# Mchengerwa kulinda maslahi ya walimu

"Kiongozi yeyote wa Serikali ambaye yuko chini yangu, yeyote bila kujali cheo chake ambaye itabainika anamuonea au kumnyanyasa mtumishi, mwalimu au aliye kwenye Sekta ya Afya au anayewajibika kwangu Kiongozi huyo maana yake hanifai.



> Katika kipindi changu kama Waziri wa TAMISEMI sitegemei kusikia manung'uniko na sitegemi kuona uonevu kwa walimu nchi nzima



WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Mhe. Mohamed Mchengerwa amesema atalinda maslahi na haki za walimu na hatapenda kusikia manung'uniko au uonevu wa aina kutoka kwa watumishi wakiwamo walimu.

Mchengerwa aliyasema hayo Jijini Dodoma kwenye mkutano Mkuu wa Umoja wa Walimu Wakuu wa Shule za Msingi nchini (TAPSHA) uliofanyika hivi karibuni.

Alisema akiwa Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais TAMISEMI hataki kusikia manung'uniko na uonevu kwa walimu na watumishi wengine na kwamba hatakuwa na huruma kwa Kiongozi atakayefanya hivyo.

"Katika kipindi changu kama Waziri wa TAMISEMI sitegemei kusikia manung'uniko na sitegemi kuona uonevu kwa walimu nchi nzima"

"Kiongozi yeyote wa Serikali ambaye yuko chini yangu, yeyote bila kujali cheo chake ambaye itabainika anamuonea au kumnyanyasa mtumishi, mwalimu au aliye kwenye Sekta ya Afya au anayewajibika kwangu Kiongozi huyo maana yake hanifai."

"Hii itashuka mpaka chini kuanzia kwa wasaidizi wangu, itashuka mpaka chini Wakuu wa Wilaya, Wakurugenzi na wengine wote, maana yangu ni kwamba tunataka kila mmoja wetu afanye kazi kwenye eneo lake akitanguliza maslahi ya Taifa letu, akitanguliza maadili ya Taifa letu akitanguliza uzalendo kwa kila mmoja wetu nadhani hii nimeeleweka vizuri."

Alisema aliwapigania watumishi wakiwamo walimu na kupandishwa madaraja na kulipwa stahiki zao akiwa Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora na kwamba ataendelea kufanya hivyo akiwa Ofisi ya Rais-TAMISEMI.

"Najua nilipokuwa Utumishi niliwapigania sana na wengi mlipanda madaraja ambao mlikuwa mmekaa miaka mingi bila kupanda madaraja. Inawezekana kuna baadhi yenu hamkufanikiwa kwa sababu ya kasoro za watendaji wetu kwenye maeneo yetu."

"Hivyo, namuagiza Katibu Mkuu TAMISEMI Adolf Ndunguru kurekebisha mara moja kasoro zilizowakwamisha baadhi ya walimu kupanda madaraja na kuhakikisha wapandishwa madaraja na kulipwa stahiki zao mara moja"

"Ujumbe wangu kwenu ni kuwaomba wakati huu nikiwa waziri wa TAMISEMI nendeni mkajivunie kabisa. Nitawalinda wale wote wanaofanya kazi kwa bidii, nitawalinda hasa."

"Niwaombe nendeni mkafanyekazi kwa bidii tunatambua kazi yenu ni kazi ya kujitolea ninawaomba sana mtangulizeni Mungu mbele kwa kila mnalo lifanya katika maeneo yenu na Serikali itahakikisha inafanya kila kinachotakiwa ikiwamo suala la kusimamia maslahi ya watumishi.

"Niwathibitishie pale ambapo Serikali inapaswa kufanya tutafanya, pale ambapo tunapaswa kuwapandisha madaraja tutawapandisha kwa namna inavyotakiwa, pale ambapo tunapaswa kusimamia masilahi tutasimamia maslahi yenu kwa nguvu zote."

Aliongeza kuwa Rais Samia Suluhu Hassan anawapenda na kuwajali sana walimu wote nchi nzima. "Niwathibitishie lile la kwenu ni la kwangu nitalibeba kama la kwangu.

# Wakuu wa Shule wasipokwe madaraka katika kusimamia miradi - Dkt. Msonde




NAIBU Katibu Mkuu (Elimu), Ofisi ya Rais-TAMISEMI Dkt. Charles Msonde amekemea kitendo cha baadhi ya Viongozi wa Halmashauri nchini kuwapoka Wakuu wa Shule jukumu la kusimamia miradi ya ujenzi wa miundombinu ya shule kwa kudhani kuwa hawana uwezo wa kusimamia miradi hiyo.

Dkt. Msonde amekemea tabia hiyo ya baadhi ya viongozi, wakati wa kikao kazi chake na viongozi wa mkoa na halmashauri kilichofanyika katika Ofisi ya Mkuu wa mkoa wa rukwa kilicholenga kufanya tathmini na majumuisho ya ziara yake aliyoifanya hivi karibuni baada ya kukagua ujenzi wa miundombinu sekta ya elimu mkoani Rukwa.

Dkt. Msonde amesema uzoefu unaonesha kuwa, popote pale ambapo Wakuu wa Shule wamepokwa jukumu lao la kusimamia utekelezaji wa miradi, miradi hiyo haijakamilika kwa wakati kama ilivyokusudiwa na Serikali.



Dkt. Charles Msonde Naibu Katibu Mkuu (ELIMU) Ofisi ya Rais TAMISEMI

> Halmashauri haitekelezi wajibu wake wa kusimamia utendaji kazi wa Mkuu wa Shule na badala yake zinatekeleza yale ambayo yanapaswa kufanywa na Kamati za Manunuzi, Kamati za Mapokezi na usimamizi wa shule wakati ni kinyume na taratibu.

"Halmashauri haitekelezi wajibu wake wa kusimamia utendaji kazi wa Mkuu wa Shule na badala yake zinatekeleza yale ambayo yanapaswa kufanywa na Kamati za Manunuzi, Kamati za Mapokezi na usimamizi wa shule wakati ni kinyume na taratibu," Dkt. Msonde alifafanua.

Dkt. Msonde ameanisha kuwa, Serikali ilipoamua kupeleka shuleni fedha za ujenzi wa miundombinu haikukosea kwani iliwapa hadhi Wakuu wa Shule kuwa maafisa masuuli, hivyo Wakuu wa Wilaya na Makatibu Tawala wa Wilaya wanaowajibu wa kuwalinda Walimu Wakuu wasipokwe majukumu yao ili kulinda jukumu walilopewa.

Amefafanua zaidi kuwa, Mwogozo wa kufanya manunuzi kwa kutumia 'Force Account' umetoa mwelekeo kwa Walimu Wakuu kwa namna ya kutekeleza majukumu yao ikiwa ni pamoja na uundaji wa kamati mbalimbali zikiwemo za manunuzi na ujenzi ambazo miongoni mwake wajumbe wanatokana na wataalam wa manunuzi na wahandisi.

Ofisi ya Rais-TAMISEMI imekuwa ikifanya ukaguzi wa mara kwa mara kwenye ujenzi na ukarabati wa miradi ya maendeleo ikiwa ni pamoja na miradi ya GPE LANES II kwa ambayo imetekelezwa kwa kushirikiana na Wadau wa Elimu (GPE) ambapo Serikali inaendelea kukarabati miundombinu ya zamani lakini pia kujenga miundombinu mipya.





# Simamieni magari yaliyotolewa kufuatilia kazi za elimu - Mchengerwa

> Maafisa Elimu fanyeni mikutano na walimu, nendeni mshuke vijijini mkatatue kero na changamotoa za walimu mara moja na zile zilizo nje ya uwezo wenu kazileteni kwetu" Alisema Mheshimiwa Mchengerwa.






HIVI karibuni Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais TAMISEMI Mhe. Mohamed Mchengerwa aliwaelekeza Wakuu wa Mikoa na Wilaya kuhakikisha wanasimamia matumizi ya magari mapya 13 yaliyotolewa na Serikali kuwa yanaleta tija ya kuwahudumia watumishi na kutatua kero za wananchi.

"Maafisa Elimu fanyeni mikutano na walimu, nendeni mshuke vijijini mkatatue kero na changamotoa za walimu mara moja na zile zilizo nje ya uwezo wenu kazileteni kwetu" Alisema Mheshimiwa Mchengerwa.

Waziri Mchengerwa aligawa magari 13 yenye thamani ya zaidi ya Shilingi Bilioni 1.8 yatakayosaidia ufuatiliaji wa masuala ya elimu msingi katika Halmashauri 13 kupitia Mradi wa Kukuza Stadi za Kusoma, Kuandika na Kuhesabu (GPE LANES II) na kuwaelekeza viongozi wa Mikoa na Wilaya kufuatilia matumizi sahihi ya magari hayo.

Aidha, Waziri Mchengerwa alisaini Mradi mpya na Wadau wa Elimu Duniani (Global Partnaship for Education) wenye afua za kutatua changamoto za walimu nchini unaojulikana kama Programu ya Kuboresha Kada ya Ualimu 'Teacher Support Programme' (GPE-TSP) wenye thamani ya Shilingi Bilioni 264 ambao utekelezaji wake utaanza baada ya kuzinduliwa rasmi na Mheshiwa Dkt. Rais Samia Suluhu Hassan tarehe 13 Machi, 2024 Sekta ya Elimu pia inamfanya Dkt. Samia Suluhu kuendelea kuimarisha mahusiano ya kimataifa na nchi nyingine na Wadau mbalimbali wa maendeleo.

Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Serikali za Mitaa Mheshimiwa Dennis Lazaro Londo alisema magari yaliyotolewa na Programu ya Kuimarisha Stadi za Kusoma, Kuandika na Kuhesabu (GPE LANES II) yatasaidia kuhamasisha utendaji kazi na utekelezaji wa kitaaluma hasa maeneo ya pembezoni kwani yatasaidia kuongeza kiwango cha ufaulu kwa wanafunzi.

Peter Fusi Afisa Elimu (Msingi) Halmashauri ya Wilaya ya Iringa alitoa shukrani kwa Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuwapatia gari kupitia Programu ya GPE LANES II kwani yeye ndiye sauti yao kwa Wadau wa Maendeleo na sasa wataweza kufika maeneo korofi kama yale yanayozunguka Mto Ruaha na Bwawa la Mtera.





# Sera mpya ya elimu, mtaala mpya kuleta mageuzi ya elimu Tanzania

SERIKALI ya Tanzania hivi karibuni ilichukua hatua ya kufanya mageuzi katika Sekta ya Elimu ili kuleta mabadiliko chanya ndani na nje ya nchi kwa faida ya Watanzania, mafanikio haya makubwa yanatekeleza Malengo ya Maendeleo Endelevu ya mwaka 2030 (SDGs) kwa kufanya Utekelezaji wa Sera ya Elimu Bila Malipo kwani elimumsingi inatolewa bure kuanzia elimu ya Awali, kidato cha kwanza hadi kidato cha nne hakuna ulipaji wa ada kama ilivyokuwa miaka michache iliyopita na hii itawezesha kila mtoto wa Kitanzania kwenda shuleni na kusoma bila kizuizi cha kulipa ada.

Pia wanafunzi wa kike wote waliokuwa wamekatishwa masomo hapo awali kutokana na kupata ujauzito na sababu nyingine wamerudishwa shuleni kuendelea na masomo na kuhakikishia Umma wa Watanzania kuwa elimu inatolewa kwa usawa bila kumbagua mtoto yeyote.

Prof. Mkenda anasema Serikali kupitia Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia imefanya mabadiliko ya Sera na Mtaala wa Elimu ili kuendana na mabadiliko ya Ulimwengu wa sasa ambapo kwa hivi sasa wanafunzi wataishia darasa la sita na watalazimika kumaliza kidato cha nne kama elimu ya lazima.

Prof. Mkenda pia anasema mkazo pia upo katika kutambua nani anafaa kuwa mwalimu, vigezo gani vitumike na aajiriwe vipi, kwani sio suala tu la ukikosa kazi mahali fulani basi kazi ya kada ya ualimu ndio inakuwakimbilio la wabovu, dhana hiyo sasa imefutika nah apo tena ili nchi iwe na walimu wanaokidhi vigezo vyote kwa ajili ya kuzalisha wataalam mbalimbali.

Aidha, Prof Mkenda anafafanua kuwa Tanzania imeanza safari ya utekelezaji wa Sera Mpya ya Elimu na Mafunzo ya Mwaka 2014 Toleo la 2023 pamoja na mitaala mipya kwa kuanza utaratibu ambao utaongeza muda wa wanafunzi kukaa shuleni kwa lazima kutoka miaka saba mpaka kufika miaka 10.

Utekelezaji wa sera, mitaala mipya inaanza na wanafunzi wa Elimu ya Awali, darasa la kwanza, darasa la tatu, kidato cha kwanza kwa wale ambao wamechukua mkondo wa elimu ya sekondari ya amali, kidato cha tano wanaotarajiwa kuanza katikati ya mwaka huu 2024 na mwaka wa kwanza katika vyuo vya Ualimu.

Dkt. Lyabwene Mtahabwa ni Kamishana wa Elimu, Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia



aliongea na Wathibiti Ubora wa shule na Maafisa Elimu Kata wakati wa kikao kilichofanyika katika Manispaa ya Morogoro hivi karibuni kuhusu mtaala mpya, na kutoa wito kwa Wataalam hao kufanya kazi vizuri na mwalimu, kuwaheshimu walimu, kuwapenda, kuwathamini pasipo kutoa maelekezo bila kuwapa elimu ya jambo lolote ikiwa ni pamoja na utekelezaji wa mitaala mipya.


Katika kikao cha Wathibiti Ubora na Maafisa Elimu Kata, Mkurugenzi Msaidizi Elimu ya Msingi na Elimu ya Awali Ofisi ya Rais TAMISEMI Bi Susan Nusu alisema, kama watekelezaji wa Sera katika ngazi ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa jukumu lao litakuwa ni kuhakikisha wanatoa ushirikiano kwa Wizara ya Elimu na Taasisi ya Elimu ili Mtaala mpya ulioboreshwa uende kuwa chachu ya mabadiliko katika Sekta nzima ya Elimu.

Mkurugenzi Mkuu wa Taasisi ya Elimu Tanzania Dkt. Aneth Komba alitoa wito kwa Wathibiti Ubora wa shule kuzingatia kwa undani mafunzo yaliyotolewa na Taasisi ya Elimu Tanzania (TET) ili kwenda kuwafundisha walimu wote kwenye Kata zao kuuelewa mtaala mpya na namna bora ya kuutekeleza kwani Maafisa Elimu Kata na Wathibiti Ubora wa shule ni wawakilishi wa Taasisi ya elimu Tanzania (TET) katika maeneo yao ya utendaji hivyo ni muhimu kusaidia kutatua changamoto zinazowakumba walimu katika shule zao badala ya kuandika taarifa ya changamoto hizo bila kusaidia katika utatuzi.

Utekelezaji wa Sera Mpya ya Elimu na Mafunzo ya Mwaka 2014 Toleo la 2023 pamoja na mitaala mipya umeanza kutekelezwa mwaka 2024 ambapo mwaka 2027 zao la kwanza la mtaala mpya kwa darasa la tatu litahitimu elimu ya msingi na kujiandaa na elimu ya lazima ya kidato cha kwanza hadi cha nne.



**Mwalimu Susan Nusu Nyarubamba Mkurugenzi Msaidizi Elimu ya Awali na Msingi Ofisi ya Rais TAMISEMI akiteta jambo na mwanafunzi wakati wa ziara ya ufuatiliaji wa Miradi ya Maendelo ya Programu ya GPE.**





**Profesa Adolf Mkenda**

> **Serikali kupitia Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia imefanya mabadiliko ya Sera na Mtaala wa Elimu ili kuendana na mabadiliko ya Ulimwengu wa sasa ambapo kwa hivi sasa wanafunzi wataishia darasa la sita na watalazimika kumaliza kidato cha nne kama elimu ya lazima.**



Dkt. Doto Mashaka Biteko



Mhe. Charlotta Ozaki Marcias

# "Serikali, Wadau nguvu moja kutekeleza Programu ya Kuboresha Kada ya Ualimu Tanzania (GPE TSP)"

HIVI karibuni Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa walifanya Hafla ya Kuzindua Programu ya Kuboresha Kada ya Ualimu 'Global Partneship for Education Teacher Support Programme' (GPE TSP) ambayo ilifanyika katika Ukumbi wa Diamond Jubilee, Upanga Jijini Dar es Salaam na mgeni rasmi alikuwa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambaye aliwakilishwa na Mheshimiwa Dkt. Doto Mashaka Biteko Naibu Waziri Mkuu wa Tanzania na Waziri wa Nishati.

Programu ya Kuboresha Kada ya Ualimu ambayo utekelezaji wake umeanza kuanzia mwaka wa fedha 2023/2024 na inatarajiwa kukamilika mwaka wa fedha 2026/2027, inakuja baada ya Serikali ya Tanzania na Sweden kukubaliana na kusaini Mkataba wa Msaada wa Dola za Marekani Milioni 84.66 sawa na Shilingi za kitanzania Bilioni 210 baada ya kukamilika kwa Programu ya GPE LANES Awamu ya Kwanza iliyotekelezwa kuanzia mwaka 2013/2014 hadi mwaka 2017/2018 na GPE LANES Awamu ya Pili iliyotekelezwa kuanzia mwaka 2018/2019 hadi mwaka 2021/2022.

Programu ya GPE LANES I ililenga kuboresha upatikanaji wa stadi za Kusoma, Kuandika na Kuhesabu (3Rs – Reading, Writing and Numeracy skills) miongoni mwa watoto walio ndani na nje ya mfumo wa shule, kwa kuzingatia zaidi watoto waliotengwa na wale walio katika mazingira magumu kufikiwa na kupata huduma lakini pia GPE LANES II iliendeleza yote ya awamu ya kwanza na kuboresha zaidi kwa kutoa Mafunzo ya Walimu Kazini (MEWAKA), ujenzi wa miundombinu ya kufundishia na kujifunzia walimu pamoja na wanafunzi, utoaji wa vifaa vya TEHAMA, kuboresha mazingira ya ujumuishi katika ufundishaji na ujifunzaji na kuwajengea uwezo viongozi waliopo katika Sekta ya Elimu nchini ili kuboresha fursa ya utoaji wa elimu jumuishi.

Katika Hafla hiyo Viongozi wa Kitaifa na Kimataifa walipata wasaa wa kutoa hotuba zao akiwemo Mheshimiwa Balozi Charlotta Ozaki Macias, Balozi wa Sweden nchini Tanzania alisema Mpango wa Kuboresha Kada ya Ualimu unalenga pia kuhakikisha upatikanaji wa takwimu sahihi za walimu, aina ya ujuzi walionao na mahali wanapohitajika walimu kwani uwepo wa walimu bora ni kichocheo cha mabadiliko katika ujifunzaji wa wanafunzi shuleni kwani walimu ni chachu ya mabadiliko katika elimu.




**Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati akiwa ameambatana na viongozi wengine akizindua Programu ya Kuboresha Kada ya Ualimu (GPE TSP).**

"Walimu ni chachu ya mabadiliko, walimu wanalo jukumu muhimu katika kuwawezesha watoto kujifunza lakini pia wazazi wanatakiwa kuwa na msukumo ili kusaidia watoto wao katika mchakato mzima wa kujifunza" alisema Balozi Charlotta Ozaki Marcias.

Balozi Macias aliongeza kuwa mkakati wa sasa wa Wadau wa Elimu Duniani (GPE) unasisitiza zaidi usawa wa kijinsia kwa watoto wote, upatikanaji wa takwimu muhimu za walimu kwa ajili ya kuwezesha mipango thabiti, kujua mahitaji na usambazaji wa rasilimali bora zinazotumika kwani hili litasaidia hata nchi ya Sweden ambayo itasaidia kufadhili kituo cha Kitaifa cha takwimu (National Data) na uandaaji wa kiunzi (tool) kitakachowezesha mgao wa walimu ili kuondokana na uhaba wa walimu katika maeneo ya pembezoni na magumu kufikiwa.

Pia Balozi Macias alisisitiza uwekaji wa kipaumbele katika upangaji na usimamizi wa walimu kama eneo muhimu la kuleta mageuzi lengo likiwa ni kuhakikisha Tanzania inakuwa na idadi sahihi ya walimu wenye ari ya kufundisha na ujuzi sahihi utakaotumika mahali sahihi lakini pia mafanikio ya wanafunzi hayawezekani bila kuwepo kwa walimu wenye ari ya kazi na ubora katika mazingira mazuri ya kujifunzia.

Balozi Macias aliishukuru Serikali ya Tanzania kwa kudumisha ushirikiano na nchi yake na kuahidi kuwa Serikali ya Sweden itashirikiana na washirika wengine wa maendeleo katika sekta mbalimbali nchini Tanzania ili kufanikisha utekelezaji wa Programu ya Kada ya Ualimu (GPE TSP) nchini Tanzania ndani ya muda uliopangwa.

Mwingine aliyepata wasaa ni Mheshimiwa Husna Sekiboko Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Elimu, Utamaduni na Michezo akimwakilisha Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. Tulia Ackson alisema matunda makubwa katika Sekta ya Elimu yameonekana katika kipindi cha Serikali ya Awamu ya Sita ya Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania lakini aliweka msisitizo zaidi kwa Serikali kuajiri walimu na kuboresha maslahi ya walimu nchini.

Sekiboko alisema maendeleo yoyote ni lazima yataletwa kupitia shule na maboresho yote yatakayofanywa kupitia Mpango wa GPE TSP Bunge litaendelea kuunga mkono utekelezaji wake na hapa alitoa angalizo kwa Watendaji na Serikali kwa ujumla kuhakikisha fedha zote zitakazotolewa kwa ajili ya utekelezaji wa Programu ya Kuboresha Kada ya Ualimu zitumike kwa malengo mahususi yaliyokusudiwa ili kuendelea kujenga imani kwa wafadhili, kutatua kero na changamoto zilizopo katika Sekta ya elimu hapa nchiuni.

Mheshimiwa Prof. Adolf Mkenda, Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia alimpongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuleta mageuzi makubwa katika Elimu nchini, hususani kukubali kufanya maboresho ya Sera na Mitaala lakini pia alisema utoshelevu wa walimu na ubora wa walimu, miundombinu na vitendea kazi ni vitu ambavyo haviepukiki na kuwa Programu ya Kuboresha Kada ya Ualimu inakuja kuongeza nguvu katika eneo hilo.

Mheshimiwa Mkenda alisema kuhusu mageuzi katika Sektya ya Elimu alisema mambo saba yanaendelea kufanyiwa kazi ambayo ni Sera, Sheria, mitaala, utoshelevu wa walimu, wakufunzi na wahadhiri, ubora wa walimu, wakufunzi na wahadhiri, ujenzi na ukarabati wa miundombinu pamoja na vitendea kazi ambavyo vyote kwa pamoja vitasaidia kuboresha elimu nchini na kwamba hadi kufikia hivi sasa mitaala imeshafanyiwa kazi na utekelezaji wake unaanza kidogo kidogo.

Hivyo, Programu ya GPE TSP iliyozinduliwa inagusa mambo yote saba yaliyotajwa kwa kutoa mafunzo ya walimu kazini (MEWAKA), kuwaandaa walimu na kuwapanga, kuwasaidia walimu, kuwajengea uwezo wao ili waweze kuwa bora zaidi, ujenzi wa nyumba za walimu na ugawaji wa vishikwambi zoezi ambalo lilifanyika nchi nzima.

Mheshimiwa Mkenda aliongeza kuwa vishikwambi vilivyogawiwa kwa walimu nchi nzima vitawasaidia walimu kupakuwa (download) vitabu kutoka Taasisi ya Elimu Tanzania (TET) vitakavyowasaidia kuboresha ufundishaji na ujifunzaji wa walimu na wanafunzi na sula hili linaendana na Sera ya Elimu na Mafunzo yam waka 2014 toleo la mwaka 2023 (Sera ya Elimu) ambayo inasisitiza sana uandaaji wa walimu, kujenga uwezo wa walimu walioajiriwa na kuwapanga walimu wapya kwa utaratibu maalum ili

**Inaendelea uk 34**




**Inatoka uk 33**

kupata walimu bora watakaoleta mageza ya elimu nchini.

Akimwakilisha Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa Mheshimiwa Mohamed Mchengerwa, Mheshimiwa Deogratius Ndejembi ambaye alikuwa Naibu Waziri (ELIMU) Ofisi ya Rais TAMISEMI alitoa salamu za Ofisi hiyo kwa kusema Serikali ipo makini katika kuhakikisha mazingira ya utoaji wa elimu yanakuwa bora na rafiki kwa makundi yote wakiwemo Watoto wenye mahitaji maalum, uboreshaji wa mazingira ya ufundishaji na ujifunzaji ambayo yameimarishwa kupitia wizara mbili za Elimu, Sayansi na Teknolojia na Ofisi ya Rais TAMISEMI na kuhakikisha kwamba ushirikiano uliopo utaendelezwa ili kuboresha Sekta ya Elimu hapa nchini.

Aidha, Mheshimiwa Ndejembi alitoa pongezi kwa Wadau wa elimu waliopo ndani na nje ya nchi na wasimamizi wa elimu lakini kwa upekee aliwapongeza walimu wote nchini kwa juhudi zao wanazozifanya katika kuhakikisha wanafunzi wanapata ujuzi, maarifa na stadi zinazotakiwa.

Akitoa hotuba ya awali kabla ya mgeni rasmi, Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete ambaye ndiye Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya Ushirika wa Kusaidia Maendeleo ya Elimu Duniani (GPE) alisema GPE iliundwa takribani miaka 20 iliyopita, mwaka 2002 na nchi zilizoendelea kiviwanda (G7) kwa lengo la kuchochea elimumsingi kwa nchi zinazoendelea hasa zilizo katika kipato cha chini, kipato cha kati na zilie zilizo katika hatua ya awali na zaidi katika kuhakikisha hakuna mtoto anayekosa elimu kwa sababu ya matatizo aliyonayo katika jamii yake.

Kikwete alisema pia GPE inafanya kazi katika nchi 89 Duniani ambapo nchi 44 zipo Afrika na mpaka sasa Dola Bilioni 6 kuboreshwa Mifumo ya Elimu Afrika, kwa Tanzania imekwisha pokea Dola Milioni 330 kuboresha elimumsingi yaani kuanzia elimu ya awali, msingi na sekondari

Alitoa pongezi kwa juhudi za Serikali ya Tanzania kwa kuleta matokeo chanya ya kuongeza idadi ya wasichana wanaomaliza darasa la saba na kujiunga na elimu ya sekondari, kuondoa marufuku kwa wasichana waliopata mimba wasiendelee na masomo (usawa wa kijinsia) na kuhakikisha kila kijana anayemaliza elimu ya msingi anapata nafasi ya kujiunga na kidato cha kwanza.

Kikwete aliyataja mafanikio ya GPE kwa Tanzania kuwa ni pamoja na kuiwezesha Serikali kuchapa vitabu 36,118,566 lengo likiwa kitabu kimoja kwa mtoto mmoja, ujenzi wa madarasa ya shule za msingi 2680, ujenzi wa madarasa ya awali ya mfano 300, ujenzi na ukarabati wa vituo vya walimu 252, ujenzi wa nyumba 64 za walimu, shule mpya 18, mabweni 15 ya Watoto wenye mahitaji maalum, ujenzi na ukarabati wa shule 13 za mahitaji maalum kwa ajili ya kuimarisha elimu nchini.

Kikwete alisema kwa mujibu wa takwimu za Dunia kuna jumla ya Watoto milioni 240 ambao wapo nje ya mfumo wa elimu na milioni 100 wapo Afrika na hata waliopo shuleni asilimia 33 hawamalizi masomo yao.

Mgeni Rasmi akimwakilisha Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Mhe. Dkt. Doto Mashaka Biteko alisema uwekezaji wowote katika elimu ni lazima umguse mwalimu kwani ndiye anayewezesha au kiongozi wa rasilimali na shughuli zote kwenye sekta zote kwa mujibu wa kazi zao.

Mheshimiwa Biteko alisema pamoja na Serikali kuwa na changamoto lukuki suala la ubora litakuwa endelevu lakini kila mwananchi kuipata elimu ni jambo la lazima, hapa anafafanua namna ambavyo Serikali ilivyofanikiwa kuongeza idadi ya wanafunzi waliofaulu kutoka shule za msingi kwenda sekondari kutoka 907,802 mwaka 2021 hadi 1,092,984 mwaka 2023 sawa na asilimia 20.4, idadi ya walimu imeongezeka ambapo jumla ya walimu 37,473 waliajiriwa, madarasa 227,383 yalijengwa kwa shule za msingi na sekondari lakini pia walimu 20,000 walibadilishiwa vyeo (recategorization) kwenda kada nyingine kuendelea na majukumu ya Serikali.

Dkt. Biteko alifafanua kuhusu udahili wa wanafunzi kujiunga na darasa la kwanza kuwa umeleta changamoto ya mahitaji ya miundombinu shuleni kwani mwaka 2023 wanafunzi wapatao 10,824,374 walijiunga na darasa la kwanza na kupelekea mahitaji ya madarasa 96,166 na inakadiriwa mwaka 2030 watadahiliwa wanafunzi 13,511,477 na mahitaji ya madarasa yatakuwa 59,418 lakini kwa upande wa sekondari wanafunzi wapatao 2,618,325 walijiunga na kidato cha kwanza mwaka 2023 na inakadiriwa mwaka 2030 wataongezeka na kufikia 3,265,321 na watahitaji nyongeza ya madarasa 16,153.

Kwa upande wa nyumba za walimu Dkt. Biteko alisema mahitaji yatakuwa makubwa zaidi kwani kwa takwimu za mwaka 2023 zipo nyumba 45,181 za walimu wa shule za msingi na sekondari ambapo mahitaji ni nyumba 35,206.

Aidha, Mhe. Biteko alisema Serikali itaendelea kuwajali walimu ambapo kwa hivi sasa pamoja na kujali maslahi yao, Serikali imeongeza bajeti ya elimu kutoka Shilingi Trilioni 4.7 hadi Shilingi Trilioni 5.7 sawa na ongezeko la asilimia 20.4 na kwamba kwa kushirikiana na Wadau wa GPE kupitia Programu ya GPE TSP itahakikisha inakamilisha na kufanikisha malengo yake kwa wakati kwa manufaa ya wananchi kama inavyotarajiwa.

Katika hatua nyingine Mheshimiwa Biteko alivitaja vipaumbele vya Serikali katika kutekeleza Programu ya Kuboresha Kada ya Ualimu (GPE TSP) nchini kuwa ni ujenzi wa nyumba za walimu kwa Halmashauri zilizopo pembezoni, kuimarisha mfumo wa motisha kwa walimu na kuwabakiza katika taaluma yao kwa kuwapa mazingira bora na kuwafanya kuwa na thamani ya kufundisha.

Pia kuwezesha mfumo jumuishi wa kielektroniki ambao utatumika kufanya upangaji wa walimu (msawazo) na hii inasaidia kuondoa changamoto ya mlundikano wa walimu katika sehemu moja lakini pia kuwezesha utekelezaji wa mpango wa ajira kwa walimu wa kujitolea

# "Serikali, Wadau nguvu moja kutekeleza Programu ya Kuboresha Kada ya Ualimu Tanzania (GPE TSP)"

> **Serikali itaendelea kuwajali walimu ambapo kwa hivi sasa pamoja na kujali maslahi yao, Serikali imeongeza bajeti ya elimu kutoka Shilingi Trilioni 4.7 hadi Shilingi Trilioni 5.7 sawa na ongezeko la asilimia 20.4.**

ambao watawezeshwa posho ya shilingi laki tatu kwa mwezi ili kupunguza changamoto ya upatikanaji wa walimu msingi shuleni ili kuimarisha mazingira ya ufundishaji na ujifunzaji.

Hali kadhalika uwezeshaji wa upimaji wa kielektroniki shuleni kwa kila hatua ya kujifunza ambayo itawawezesha walimu kufanya rejea, pia kutakuwa na ujenzi wa vituo vya walimu (TRC) ambavyo vitawekewa samani na vifaa vya kielektroniki vitakavyowezesha mafunzo ya walimu kazini (MEWAKA) na kukuza utumiaji wa teknolojia ili kuendana na mabadiliko ya TEHAMA Duniani.

Matarajio mengine ni ununuzi wa zana na vifaa visaidizi vya ufundishaji na ujifunzaji kwa wanafunzi wenye mahitaji maalum kwa walimu, wakufunzi na walimu tarajali wanaofundisha wanafunzi wenye mahitaji maalum.

Mwisho ni kutoa ufadhili wa masomo kwa walimu wanaofundisha wanafunzi wenye mahitaji maalumili kuendelea kutoa elimu jumuishi na kufikia malengo ya kutoa elimu bora bila kumwacha mtoto yeyote anayestahili kupata elimu apate elimu.

Mheshimiwa Biteko alitoa maagizo kwa Ofisi ya Rais TAMISEMI na Wizara ya Elimu, Sayanasi na Teknolojia kuanzisha siku ya mwalimu nchini ili kutoa motisha kwa walimu kama sehemu ya kutambua mchango wao katika elimu ambapo zawadi mbalimbali zitolewe pamoja nav yeti na tuzo kwa walimu waliofanya vizuri na kuwa mfano kwa wenzao.

Baada ya kutoa hotuba yake kwa niaba ya Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan, Mheshimiwa Dkt. Doto Mashaka Biteko Naibu Waziri Mkuu wa Tanzania alipata wasaa wa kuzindua Programu ya Kuboresha Kada ya Ualimu (GPE TSP) ambayo utekelezaji wake umeanza kuanzia mwaka wa fedha 2023/2024 na unatarajiwa kukamilika mwaka wa fedha 2026/2027.





**Katibu Mkuu Wizara ya Fedha ambaye pia ni Mlipaji Mkuu wa Serikali, Dkt. Natu El-Maamry Mwamba akisaini Mkataba wa Msaada wa fedha Shilingi Bilioni 210 kutoka Mfuko wa Elimu Duniani (GPE) na Balozi wa Sweden nchini Tanzania, Mhe. Charlotta Ozaki Macias Jijini Dar es Salaam.**



Catalysing Education
Sector as One